

HALMASHAURI KUU YAWATEUA:

Salim Katibu wa Tume ya Ulinzi na Usalama

Nyang'anyi mjumbe wa Kamati Kuu

Na Mwandishi Wetu

Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kauli moja jana ilimteua mjumbe wa Kamati Kuu, Ndugu Salim Ahmed Salim, kuwa Katibu wa Tume ya Ulinzi na Usalama na Ndugu Mustafa Nyang'anyi kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu.

Ndugu Salim, ambaye pia ni Waziri Mkuu, anachukua nafasi iliyoachwa wazi na hayati Edward Moringe Sokoine ambaye pia alikuwa Waziri Mkuu. Vilevile Ndugu Nyang'anyi anajaza nafasi iliyoachwa wazi na Ndugu Sokoine. Hayati Sokoine alifariki kwa ajali ya gari Aprili 12 mwaka huu wakati akisafiri kutoka Dodoma kuja Dar es Salaam.

Taarifa ilivotolewa mjini Dar es Salaam na Idara ya Uenezi na Ushirikishaji umma ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ilieleza pia kuwa katika kikao cha jana chini ya Mwenyekiti wa Chama, Mwalimu Nyerere, Halmashauri Kuu ya Taifa, pia ilifanya uteuzi wa mwisho wa majina ya wanaogombea nafasi ya mwenyekiti wa Chama mkoa wa Kigoma.

Majina ya wagombea hao yaliyopitishwa ni Ndugu Bahingayi Newman Malekela (39), Ndugu Aaron Ntirubayejo Mpambije (39), Ndugu Samson Mahuyo Mayingo (41), Ndugu Clement Holalo Ndayeza (44), Ndugu Fridberti Bangayilubusa Nsazugwanko (41), Ndugu Stanislaus Lulikela Ntatiye (48) na Ndugu Charles Rugajo Rugiga (56).

Pia imefanya uteuzi wa mwisho wa majina matatu ya wanaogombea nafasi ya Mbunge wa Taifa mkoa wa Kagera. Majina hayo ni Ndugu Peter E.C.S. Gwasa (47), Ndugu Daudi Eliakim Kahunya (46) na Novati S. Rutageruka.

Vile vile Halmashauri Kuu ya Taifa imechukua hatua za nidhamu dhidi ya Ndugu Joseph Seleli, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tawi la Igunga, mkoa wa Tabora, kwa kukiuka miko ya Gongoni na dhidi ya wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Tawi la Muambe, wilaya ya Mkoani, Kusini Pemba kwa kupokea rushwa.

Wajumbe waliachishwa uongozi ni Ali Khamis Juma, Mwenyekiti wa Tawi Makame Tabir Silima, Katibu wa Tawi; na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi Kombe Ah Vuai, Sharif Nahoda Chande, Sheria Soud Sharia, Iddi Faki Makame, Haji Faki Makame, Mahmoud Mshenga Adibu, Kombo Ussi Wadi na Nehodhi Faki Silima.

Kwa mjiibu wa taarifa hiyo ya Idara ya Uenezi, Halmashauri Kuu ya Taifa ilishamtukuza kazi katibu wa tawi hilo, Ndugu Silima kwa makosa mengine ya wazi wa fedha za tawi hilo.

Ndugu John S. Bahche, aliyekuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa wa Mwanza na Mkuu wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya Sekretarieti ya Mkoa amechishwa uongozi kwa udanganyifu na kukiuka niadili ya Chama.



Ndugu Salim

Katika kikao hicho, Halmashauri Kuu ya Taifa pia ilipokea taarifa ya mkutano wa Umoja wa Vyama vya Kioshalioti Duniani uliofanywa Arusha, Septemba makozi. APO kuunga mkono nchi mbele na vyama ANC cha Afrika, kutoa nafasi kwa vyama cha Nchi, kutokana na mkutano huo wa kuhurua hali ya kusini mwa Afrika na kuweka wazi msimamo wa kuondolea kuunga mkono vyama vya ukombozi na nchi za mistari wa mbele katika ukombozi wa kusini mwa Afrika, mkutano huo pia ulitoa fursa kwa Chama Cha Mapinduzi kuvielewa na kujenga uhusiano na vyama vilivyohudhuria na kushiriki katika mkutano huo.

Kikao cha Halmashauri Kuu kinakomaa leo.